# UMOJA WA WAZAZI TANZANIA
# (JUMUIYA YA CCM)
# SHULE YA SEKONDARI WARI

**Simu:0745 777 015 /0788 438 341**
**0736 438 341/0757 656 994**
**Barua pepe:** warisecondary@gmail.com
**Tovuti:** www.warisecondary.ac.tz

**Barua zote zitumwe kwa**
**Mkuu wa Shule,**
**S.L.P 1988,**
**MOSHI-TANZANIA**
**Tarehe: 28/10/2024**

**FORM FIVE APPLICATION FORM-2025**

## A. COMBINATIONS OFFERED

Wari Secondary School offers the following combinations in **'A'** Level: -

| PCB | PCM | PGM | CBG | EGM | HGE |
|---|---|---|---|---|---|
| Physics<br>Chemistry<br>Biology | Physics<br>Chemistry<br>Mathematics | Physics<br>Geography<br>Mathematics | Chemistry<br>Biology<br>Geography | Economics<br>Geography<br>Mathematics | History<br>Geography<br>Economics |

## B. QUALIFICATIONS FOR BEING SELECTED

In order to qualify for Form V at Wari secondary school the following conditions must be fulfilled:

1. Applicant must have obtained at least credits in his/her Form IV Certificate of Secondary Education Examination (**CSEE**). Admission will be offered to those with at least total of ten (10) points from subjects contained in their combination.
2. Return the filled in application form to the center you collected it or directly to the school before 5th February 2025.
3. The applicant must pass an interview that will be conducted on **08th February 2025** and **1st March 2025** at **Wari secondary school, Kibo Secondary School** and **Msimbazi Center-Dar es Salaam**.

## C. ATTACHMENTS.

The following items should be attached to the filled in form:

a) Original and photocopy of the student's Ordinary level examination Results Slip (we will keep the photocopy and return the original).
b) Two latest passport size of the student.
c) A copy of the student's Birth Certificate.

**NOTE**

a) You should pay Tsh**.40, 000** non-refundable application fee through the given CRDB Account Number.
   A/C Number: **0150626495400**
   Name of Account: **ST. THOMAS AQUINAS FOUNDATION.**
b) This form can also be downloaded from our website (http://*warisecondary.ac.tz)*.
c) Attach the bank pay – in slip to the filled in application form as evidence of payment. Application form that will not be attached by such evidence shall not be considered.

(PLEASE USE BLOCK LETTER) ***Receipt Number***

1. Student's full name as it was registered in Form IV National Examination (CSEE)

   First name: ____________________ Middle name __________________Surname_____________

| **PHOTO** |
|---|
| Recent Passport size |

Sex (Please put a Tick √) Male......... Female...........

2. Student's Date of Birth: Day: ____ Month: ____ Year: ______ Place of Birth: ________________
3. Religion: ______________ Denomination: __________________Nationality ________________
4. Student's Home Address: P.O. Box ______________________________________________
5. Name of the Secondary School where student attended: _______________________
6. CSEE Centre No. ____________ Candidate's No. _____________Year Completed_____________
7. Type of 'O' level school (Please Tick Two): -

   Boarding ☐ Day ☐ Co- education ☐ Single Sex ☐

8. Fill subjects' grade obtained at O'Level as indicated in the table below: -

| **Subject** | **History** | **Geography** | **Physics** | **Chemistry** | **Biology** | **Mathematics** | **Commerce** | **B/Keeping** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Grade** | | | | | | | | |

9. O' Level results: Division: __________________________ Points: _________________________________
10. Combination the student is applying for: Please indicate 1 for first choice and 2 for the second choice.

| **CBG** | **EGM** | **PCB** | **PCM** | **HGE** | **PGM** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |

11. Number of brothers/ sisters of the applicant studying at Wari __________________________________________
12. Father's (Male Guardian's) Name _________________________________________________________

    Phone No: ___________________________, ____________________ Email _____________________________
13. Mother's (Female Guardian's) Name: __________________________________________________________

    Phone No: _______________________, ________________________ Email _____________________________
14. Area where the family lives: Region ________________ District _________________ Location: _____________

Declaration: If it is discovered that any of the above information is false, I will forfeit my place.

Name of Student __________________________ Signature __________________ Date ____________________

Name of Parent or Guardian _______________________ Signature __________________ Date ______________

You are warmly welcome to Wari Secondary School.

_____________________

STEPHEN MOSES LUHENDE

**HEAD OF SCHOOL**

**UMOJA WA WAZAZI TANZANIA**
**(JUMUIYA YA CCM)**
**SHULE YA SEKONDARI WARI**

**Simu:0745 777 015 /0788 438 341**
**0736 438 341/0757 656 994**
**Barua pepe: warisecondary@gmail.com**
**Tovuti: www.warisecondary.ac.tz**

**Barua zote zitumwe kwa**
**Mkuu wa Shule,**
**S.L.P 1988,**
**MOSHI-TANZANIA**
**Tarehe: 28/10/2024**

---

## VIGEZO NA MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI WARI.

Mzazi mwenye nia ya kuleta mtoto wako kusoma shule ya sekondari Wari hauna budi kusoma, kuelewa na kuzingatia vigezo na masharti yaliyoainishwa kwenye fomu hii na mwisho kusaini kuonesha nia ya dhati ya kumsomesha mtoto wako katika shule hii. Mzazi utapaswa kuzingatia masharti yote kwa kipindi chote ambacho mwanao atakuwa shuleni.

**A. LENGO LA SHULE: Shule ya sekondari Wari** ni ya mchanganyiko inayomilikiwa na Jumuiya ya Wazazi, yenye lengo la kutoa elimu kwa wavulana na wasichana wa Kitanzania waishio maeneo ya **Wari ndoo** na nchi **nzima kwa ujumla.** Hivyo, wanaojiunga na shule hii ni wasichana na wavulana wa Kitanzania wenye dhamira ya kupata malezi yenye lengo la kuwawezesha kukua kiakili, kimwili na kiroho ili kuitumikia jamii yao na nchi nzima kwa ujumla. Shule inaendeshwa kwa kufuata misingi ya kikatoliki ingawa wanafunzi huchaguliwa na kupata nafasi bila kujali dini au dhehebu la mwanafunzi au familia anakotoka. Shule hutoa nafasi kwa kuangalia kigezo cha ufaulu tu katika mtihani wa Taifa kidato cha nne pamoja na mtihani wa usaili (interview) ambao hufanyika **shuleni Wari Sekondari**, **Kibo Sekondari** pamoja na **Msimbazi Center-Dar es Salaam.**

**B. KUJIUNGA NA SHULE:** Wazazi wa wanafunzi wenye lengo la kujiunga na shule ya Sekondari Wari hawana budi kuzingatia mambo yafuatayo: -

(i) Kuwa elimu ni haki ya kila mtoto wa Kitanzania, msichana au mvulana aliye nyumbani ana haki sawa ya kupata elimu katika shule hii kama zilivyo shule zingine.

(ii) Kuwa ili mtoto aweze kupata nafasi ya kusoma katika shule hii, ni lazima awe amemaliza kidato cha nne ndipo anakua na sifa ya awali ya kujiunga na shule kwa kidato cha tano.

(iii) Kwa mtoto anayeomba kujiunga na shule hii, ni lazima awe na ufaulu wa daraja la I- III kwa kidato cha nne na kupata kuanzia walau point 10 (CCD) katika masomo yake ya tahasusi (combination) pamoja na ufaulu wa mtihani wa usaili (interview).

(iv) Kila mtoto anayetaka kujiunga na shule hii atalazimika kuchukua fomu maalumu ya kujiunga. Fomu hiyo hutolewa na shule na huwekwa katika vituo mbalimbali vya mawakala wetu. Kila mzazi au mtoto atalazimika kuijaza kwa utaratibu uliowekwa na kufuata mwongozo ulio katika fomu hiyo. Ikumbukwe kuwa kushindwa kuchukua fomu hii kunafanya mwanafunzi kutopewa nafasi ya kujiunga na shule.

(v) Mwanafunzi atakaekuwa amekidhi kigezo **B(iii)** hapo juu ana nafasi ya kuchaguliwa kujiunga na shule hii.

(vi) Kwa watoto watakao chaguliwa na shule watapigiwa simu ya kuwafahamisha juu ya kuchaguliwa kwao na kuwapa taratibu za awali za kujiunga na shule. Wale tu watakaothibitisha kuja ndio watakaopewa nafasi. Hii hufanyika hivyo ili kuwa na uhakika wa moja kwa moja kwa kuongea na wazazi ili wao wenyewe wathibitishe nia hiyo. Kwa wale ambao wataonesha mashaka au kukiri kupata nafasi katika shule nyingine, basi nafasi zao kutolewa kwa watoto wengine.

(vii) Kutakuwa na malipo ya awali kwa wanafunzi wote ambao watachaguliwa kujiunga na shule. Fedha hii ni ya lazima na hutakiwa kulipwa ndani ya kipindi cha wiki mbili baada ya kupigiwa simu ya kutaarifiwa kupata nafasi ya mtoto husika. **Ikumbukwe kuwa fedha hii ni sehemu ya ada, na hutumika katika kumwandikisha mtoto** na kumfanyia **maandalizi ya awali.** Baada ya kipindi hicho kupita, kwa wale wote ambao watakuwa wamefanya malipo hayo ndio watakaowekewa nafasi, na wengine wote ambao watakuwa wameshindwa kwa namna moja au nyingine kufanya malipo hayo, basi watakua wamejipotezea nafasi zao wenyewe.

(viii) Wazazi waliolipa fedha ya malipo ya awali ndio watakaopata barua ya **maelezo ya kujiunga (joining instructions).** Barua hizi hutolewa na shule kwa wazazi kupitia vituo mbalimbali kama **Moshi Bookshop karibu na Benki ya mkombozi**, **Moshi Christian Bookshop**, **Msimbazi Center- Dar- es Salaam**, **Wari** Sekondari na **Kibo** Sekondari.

## C. ADA NA MICHANGO MINGINE.

Shule ya Secondari Wari ni shule ya binafsi. Kwa maana hiyo shughuli zote za shule hutegemea ada na michango kutoka kwa wazazi ili kuweza kujiendesha. Ulipaji wa ada na michango mingine kwa wakati hurahisisha shughuli zote za shule zikiwemo za maendeleo na kitaaluma. Kwa maana hiyo wazazi wote wenye watoto shuleni au ambao watapenda watoto wao wajiunge na shule ya Wari wanapaswa kuelewa kuwa **ADA NA MICHANGO** yote ya shule hupendekezwa na shule na kuidhinishwa na bodi ya shule. Kwa maana hiyo, kila mzazi au mlezi anapaswa kuelewa kuwa atatakiwa kulipa ada na michango mingine kwa kufuata utaratibu wa wakati husika ambao pia hutolewa na shule kupitia barua rasmi kutoka kwa Mkuu wa Shule. Wazazi wakumbuke kuwa ada na michango hiyo hulipwa **KWA AWAMU MBILI TU KWA MWAKA, YAANI MARA MOJA KWA KILA MUHULA**. Kwa maana hiyo, kila mzazi anapaswa kufahamu kuwa:-

(i) Ada na michango mingine siyo jambo la hiari. Ni jukumu la lazima kwa mzazi yeyote anayetaka mwanae asome katika shule hii.

(ii) Kutakuwa na ulipaji wa ada na michango mingine kama sharti la lazima kwa mwanafunzi yoyote anayekuja Wari. Ada na michango hii hulipwa kabla ya mwanafunzi kuja shuleni na siku ya kufungua shule mwanafunzi atapaswa kuwasilisha slip ya benki ya malipo aliyofanya kisha naye atapewa stakabadhi ya shule ikionesha malipo aliyofanya.

(iii) Kwa wazazi au walezi ambao watashindwa kufanya malipo ya ada na michango mingine kwa wakati, watatakiwa kubaki na watoto wao nyumbani hadi pale watakapofanya malipo hayo, ndipo wataruhusiwa kuwaleta watoto wao shuleni.

(iv) Shule haitakuwa na uwezo wa kumvumilia au kumgharamia mwanafunzi ambaye mzazi wake atashindwa kumlipia ada. Kwa maana hiyo, mzazi atakaeshindwa kutimiza sharti la ulipaji wa ada na michango mingine kwa wakati itakuwa jukumu lake kumtafutia mwanae shule nyingine.

## D. TARATIBU ZA MAISHA YA SHULE:

Shule ya sekondari Wari ni Taasisi binafsi inayomilikiwa na Jumuiya ya Wazazi wa **CCM** na inayoendeshwa kwa kushirikiana na **ST. THOMAS AQUINAS FOUNDATION** inayofuata misingi ya kikatoliki katika malezi ya wanafunzi wawapo shuleni. Kupitia malezi haya watoto wote na jumuiya nzima hufanywa kuwa kama familia moja yenye malengo ya kusaidiana, kutembea pamoja na kuwa na ratiba moja ili kuimarisha ufanisi. Ikumbukwe kuwa shule haimbadilishi mtoto dini yake isipokuwa haya ni malezi ambayo wote watapaswa kuyafuata muda wote wawapo shuleni. Lakini pia: -

(i) Sehemu kubwa ya tabia ya mtoto hujengwa nyumbani. Malezi ya mtoto yanapaswa kuendana sana na tabia anazojengewa na wazazi au walezi wake tokea akiwa nyumbani. Kwa maana hiyo, tunategemea ushirikiano mwema katika kumlea mwanao wakati akiwa shuleni kwa ushirikiano mzuri toka kwa mzazi au mlezi. Mlezi mwema hutoa mtoto mwema kitabia.

(ii) Muda wote mtoto akiwa shuleni, atalazimika kuonesha nidhamu na adabu ya hali ya juu, na endapo ataenda kinyume na miongozo anayopewa, basi hatua kali itachukuliwa dhidi yake kulingana na kosa alilofanya.

(iii) Mzazi atakaeleta mwanae shuleni, anatakiwa kukubaliana na masharti ya kuwa tayari wakati wote kushirikiana na shule katika masuala yote yahusuyo mtoto ikiwa ni pamoja na **NIDHAMU NA TAALUMA** na kutoa ushirikiano unaostahili.

(iv) Mzazi anatakiwa kuwa tayari kumkabidhi mwanae na ataishi kwa kufuata taratibu zote zilizopo shuleni na kuwa atamhimiza mwanae kuishi kwa kufuata kikamilifu sheria za shule.

(v) Itakapolazimu kumchukulia mtoto hatua ya kumwondoa shuleni kwa sababu yoyote ile, mzazi atakubali kushirikiana na shule bila kumwathiri mtoto kisaikolojia.

**E. MAHALI SHULE ILIPO NA JINSI YA KUFIKA**

Shule ya Sekondari Wari ipo Mkoa wa Kilimanjaro Wilaya ya Hai, Tarafa ya Machame, umbali wa kilometa ishirini na tano (25) kutoka Manispaa ya Moshi.

Kwa unayetoka Moshi mjini kwa usafiri wa umma utapanda daladala (Hiace) za kuja machame na kushukia kituo cha POSTA-MACHAME kilicho karibu na kituo kidogo cha TANESCO. Kwa unayekuja kupitia njia ya Arusha utashukia barabara ya Machame
(MACHAME ROAD) kisha kupanda daladala za kuja machame na kushukia kituo cha POSTAMACHAME. Unayetumia usafiri binafsi kupitia Moshi mjini au Arusha utakuja mpaka MACHAME ROAD na kuifuta barabara ya lami mpaka POSTA-MACHAME.

**UTHIBITISHO WA MZAZI/ MLEZI.**

Mimi …………………………………….. Mzazi wa …………………………………………... ambaye anaomba kujiunga kidato cha ………………… katika shule ya sekondari Wari, nakiri kusoma na kuelewa vigezo na masharti na sahihi yangu hapa chini inathibitisha kukubali kwamba nitafuata vigezo na masharti yaliyowekwa na shule kwa lengo la kuimarisha malezi, usimamizi, pamoja na uwajibikaji katika kusimamia elimu ya mwanangu.

SAHIHI..................................................TAREHE..........................................

**Wako katika ujenzi wa Taifa**

**…………………………..…….**

**STEPHEN MOSES LUHENDE**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
S. L. P. 1988 MOSHI
WARI SEKONDARI